# EE BABA MIKONONI MWAKO.

*By: Michael Shija*
*28/03/2017*
*Bahi*

IJUMAA KUU
WIMBO WA KATIKATI




01.Nimekukimbilia wewe Bwana,
Nisiaibike milele
Kwa haki yako unipo-nye/
Mikononi mwako mwako naiweka Roho yangu,
Umenikomboa, Ee Bwana Mungu wa kweli

02. Kwa sababu ya watesi wangu nimekuwa laumu,
Naam, hasa kwa jirani za- ngu/
Na kitu cha kutisha kwa rafiki zangu,
Walioniona njiani walinikimbia

03. Nimesahauliwa kama mfu asiyekumbukwa,
Nimekuwa kama chombo kilichovunji- ka/
Maana nimesikia masingizio ya wengi,
Hofu ziko pande zote

04. Lakini mimi nakutumaini wewe Bwana,
Nimesema wewe ndiwe Mungu wa- ngu/
Nyakati zangu zipo mikononi mwako,
Uniponye na adui zangu, nao wanaonifuatia

05. Umwangaze mtumishi wako,
Kwa nuru ya uso wa- ko/
Uniokoe kwa ajili ya fadhili zako,
Iweni hodari, mpige moyo konde,
Ninyi nyote mnaomgonja Bwana.